Mafundisho Ya Namna Nyingine Nyingine Na Ya Kigeni

na

J. D. Logan

Mafundisho Ya Namna Nyingine Nyingine Na Ya Kigeni

na

J. D. Logan

Novemba 5, 2011

Mafundisho Ya Namna Nyingine Nyingine Na Ya Kigeni

Waeb. 13:9

"Msichukuliwe na mafundisho ya namna nyingine nyingine na ya kigeni; maana ni vizuri moyo ufanywe imara kwa neema wala si kwa viakula ambavyo wao waliokwenda navyo hawakupata faida."

Neno "kigeni" inatafsiriwa na kamusi ya Strongs kama xenos, mara 3581 – "kigeni (washa, mgeni, au mkuyu, adithi)".

Paulo anazungumzia nini hapa? Je alikuwa anamaanisha mafundisho ya kigeni inayofundishwa katika ulimengu?

Tunaujuzi wote wa mafundisho ya kigeni yanayofundishwa na wale wlioko katika ulimwengu – wale waliokataa mpango wa Mungu wa wokovu. Lakini ni swala tofauti kupitia mafundisho ya namna hii na wale walioko katika "nyumba ya imani".

Leo hii tunakumbana na mafundisho ya "kigeni" ambayo katika madhara yanapingana na ujumbe wa kweli wa injili. Ni muhimu kwamba tuilete hii katika mtazamo wa injili, kwamba wote waweze kuuona ukweli na kwamba wasije wakapotoshwa.

Hivi karibuni, tumearifiwa kwamba mafundisho ya Yesu katika "injili" nne (Mathayo, Marko, Luka na Yohana) si mafundisho ya na kwa faida ya kanisa, lakini kidogo inawekwa kwa Wayahudi katika wakati wa mwisho wa kizazi cha Musa.

Wazo hili limekuwa likitazamwa mara kwa mara katika mifumo tofauti kama vile, "injili nne (kama ilivyoonyeshwa) si sehemu ya Agano Jipya, bali ni vitabu vinne vya mwisho vya Agano la Kale.

Wengine wanasisitiza, "injili ilianza siku ya Pentekoste: hivyo basi chochote alichofundisha Yesu kabla ya wakati huu alikuwa anazungumzia tu Wayahudi.

Haya yote ni mambo tofauti tofauti ya nadharia hiyo iyo.

Kitu kimoja ambacho nimegundua katika hili ni kwamba mafundisho ya "kigeni" maranyingi zinaegemea katika "ajenda" ya mkosoaji. Kama mmoja akifikiria fundisho fulani, ni bora kufanya mahusiano yote ya kimandiko ili kwamba iweze kuingiliana vizuri. Hii kwa ujumla inajenga swala la kuumbuka kwa neno la Mungu.

Kazi Ya Yesu Ya Kidunia

Yesu alikuja kufanya mapinduzi! Si mapinduzi ya damu na machafuko, bali ya mioyo na mawazo ya kibinadamu.

Kwa wale wanaokaa gizani (katika swala, Wayahudi) alileta "nuru mkuu" (Math. 4:16). Nuru huo mkuu ilikuwa injili. Hii ilitokea mwanzo wa huduma yake, mara ikafuatia majaribu yake na Shetani. Tafadhali zingatia Luka 4:16-21.

Yesu alifundisha katika Sinagogi kule Nazareti kutoka katika Nabii Isaya, "*Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, na vipofu kupata kuona tena, kuwaacha huru waliosetwa.*" Hakika, alikuwa anahubiri mafundisho yenye utofauti ambayo watu hawa hawakuwahi kusikia kabla!

Sasa angalia mustari wa 21, "*Akaanza kuwaambia, leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu.*"

Yesu anasema nini? Kirahisi weka, "Leo inaanza mwanzo wa injili yangu". Mtu ye yote anaweza kuwa na shauku juu ya hili?

Marko 1:1 inaeleza, "*Mwanzo wa injili ya Yesu Kristo Mwana wa Mungu"* inaanza na kutimizwa kwa unabii wa Isaya (40:3). Hii pia ili rudiwa na Malaki (3:1) katika mwisho wa maandishi ya Agano la Kale. Kulingana na Marko, kuja kwa Yohana mbatizaji ilionyesha mwanzo wa injili ya Kristo.

Lakini huu ulikuwa ni mwanzo wa "habari njema" ya Kristo. Imezungumzia kuja kwake na matukio ambayo yangetokea juu ya mafundisho yake.

Yesu alipohubiri katika Sinagogi kule Nazareti ilionyesha mwanzo wa injili yake (mafundisho).

Tunatambua kwamba Yesu alikuwa hafundishi marudio ya sheria ya Musa, bali mafundisho yote mapya. Angalia Yohana 1:17, "*Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristo.*" (NIV) Hii inaonyesha zaidi ya kivuli cha mashaka ulinganifu kati ya "Sheria" na mafundisho ya Yesu.

Pia, tafadhali angalia: Yesu alisema (Yohana 5:45-47), "*Msidhani ya kwamba mimi nitawashitaki kwa Baba; yuko anayewashitaki, ndiye Musa, mnayemtumaini ninyi. Kwa maana kama mngalimwamini Musa, mngeniamini mimi; kwa sababu yeye alindika habari zangu. Lakini msipoyaamini maandiko yake, mtayaamini wapi maneno yangu?* Angalia ulinganifu kati ya vitu viwili hivi!

Kwa sababu ya **brevity**, hebu tufuate mageuzi ya injili kwenda mwishoni mwa kazi ya Yesu. Yesu anaeleza (Math. 24:14), "*…injili hii ya*

ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote …", ikimaanisha "agizo kuu" waliopewa mitume (Marko 16:15-16).

Yesu hakufunua sharti la injili kwa ujumla wakati wa kazi yake kwa sababu hawakuwa tayari kuupokea. Hivyo aliongea nao kwa mifano. Luka 8:10 inatufundisha, "*…Kwenu ninyi* (mitume) *mmepewa kufahamu siri* (siri: 3466 – siri au siri kupitia wazo la ukimya inayohamishwa katika kuhusisha miiko ya kidini) *ya ufalme wa Mungu: lakini kwa wengine ni kwa mifano; ili kwamba wanapotazama wasiweze kuona, na kusikia wasiweze kuelewa.*"

Haijaonyeshwa katika mafundisho yote ya Yesu, au hiyo ya mitume, zaidi "hiki" au "kile" injili.

Vivyo hivyo, wengine wanawezaje kusisitiza kwamba hivi vitu vilivyofundishwa na Yesu havina uhusiano kwa Wakristo leo? Kweli, kwa nini sasa Wakristo leo wanaongozwa?

Baadhi wanasisitiza, "injili ilianza wakati wa Pentekoste na lazima tuongozwe tu na maandishi hayo yaliyokuja baadaye.

Kwa hili naweza kujibu: Kwa hiyo tunakuta injili MBILI katika Agano Jipya? Moja ilifundishwa na Yesu wakati wa kazi yake na nyingine wakati wa Pentekoste na hapo baadaye? Hiki ni kioja sana kufikiria.

Hebu na tuifikirie kwa muda. Kama Yesu alifundisha fundisho moja na akaiita "injili hii", lakini mitume walifundisha kingine siku ya Pentekoste, tunalazimiswa na maantiki katika hitimisho lisilowezekana.

Tafadhali zingatia muda uliohusiku.

Yesu aliwaamuru mitume (siku 50 kabla ya Pentekoste) to "*…Enendeni ulimwengu mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe.*" (Marko 16:15). Kawaida, hii ingeweza kuboresha mpangilio wa muinjilisti wa siku 50 kwa *"mataifa yote"* (Math. 28:19) na "*Kwa kila kiumbe"* (Marko 16:15).

Baada ya kumaliza hii (siku 50, bila kuzidi) wangeweza kuanza mpangilio mwingine wa kuhubiri, mafundisho mengine, injili nyingine wakati wa Pentekoste. Na kwa nani wangeweza kwenda? Tayari walishakwenda katika "ulimwengu wote" wangeweza kuhimiza hatua zao na kurudia kufanya uinjilisti katika ulimwengu kwa fundisho linguine? Hii ni swala lisiloaminika sana na kufikiria!

Badala ya hili ambayo si mafundisho ya kimaandiko, tunapaswa kushawishiwa na Paulo, huyo mwandishi wa injili na mhubiri. Aliandika, "*Kwa maana ndugu zangu injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha siyo ya namna ya kibinadamu. Kwa kuwa sikuipokea kwa mwanadamu wala sikufundishwa na mwanadamu, bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo.*" (Wagal. 1:11-12).

Lakini baadhi wanasisitiza kwamba Kristo “aliifunua” kwa Paulo kwa sababu ilikuwa ni mpya; haijawahi kufundishwa kabla. Hii haiku hivyo. Paulo hakuishi na kutembea na Yesu. Alijitangaza kuwa “*…aliyezaliwa si kwa wakati.*” (1 Wakor. 15:8). Hivyo Paulo hakuwa na kumbukumbu ya “*Na kuwa kumbusha yote niliyowaambia.*” (Yohana 14:26), kama ilivyokuwa kwa mitume. LAKINI HAKUNA SEHEMU NYINGINE POPOTE AMBAPO PAULO ALISEMA KUWA NI INJILI NYINGINE!

Lakini vipi kuhusu tukio ambalo Yesu anaongelea Sheria ya Musa? Je hii ilikuwa ni injili yake?

Niliyachunguza maandiko kwa makini na kufikia hitimisho. Waandishi, Mafarisayo, madaktari, wanasheria, wakuu wa makuhani, nk. Kimsingi walimchanganya Yesu wakati wa kazi yake hapa duniani na maswali kuhusiana na maandiko yanayochanganya katika Sheria. Kusudi lao lilikuwa dhahiri; kumchanganya Yesu na kumvuruga ili kwamba mashitaka yawe juu yake. Alilazimishwa kufunua uongo wao na kutokuwaambia neno lolote na kushituliwa, mwisho kuwalazimisha kuingia katika uongo na ushahidi wa uongo kumdhihirisha mbele ya sheria.

Lakini hii haikuwa mafundisho yake; ilikuwa tu ni mkanganyiko.

Kwamba wote tuweze kujua kile ambacho kilimsababisha Yesu aje ulimwenguni kuleta kwa wanadamu, hebu kidogo twende katika maneno ya Kristo.

- Luka 21:33, “*…Neno langu halitapita kamwe.*”
- Yohana 6:63, “*…maneno ninayowaambia ni roho tena ni uzima.*”
- Yohana 6:68, “*…haya ndiyo maneno ya uzima wa milele.*”
- Yohana 14:23, “*…mtu akinipenda atalishika neno langu…*”
- Na maneno ya Paulo, mtume (Wakol. 3:16), “*Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu…*”
- Na mwisho, katika maneno ya Paulo, 1 Tim. 6:3-4, “*Mtu awaye yote akifundisha elimu nyingine, wala haya kubali maneno yenye uzima ya Bwana wetu Yesu Kristo, wala mafundisho yapatanayo na utauwa, amejivuna; wala hafahamu neno lo lote; bali anawazimu wa kuwazia habari za maswali, na mashindano ya maneno, ambayo katika hayo hutoka husuda, na ugomvi, na matukano, na shuku mbaya.*”

Ninauliza, tunapata wapi “maneno ya Yesu”? Tafuta katika injili zote nne na pale utayapata. Kama hatuyapingi, au kufundisha kivingine, karibia hatujui chochote na tunapingana na kusababisha maneno ya upuuzi ambayo hayana uthamani wa kweli kuhusu uzima wa milele.

Kuna mengine mengi ambayo yanaweza kusemwa kutoka katika maneno ya Kristo na mitume wake, ila muda hauta ruhusu. Hebu na tuziepuke mafundisho haya ya uongo kwa sababu tu zinawagawanya wafuasi wa Bwana wetu.

Na upendo kwa ndugu wote,

J D Logan